

BENKI KUU YA TANZANIA

TAARIFA KWA UMMA



UTEKELEZAJI WA AGIZO LA KUZUIA HUNDI ZA ZAIDI YA MILIONI KUMI KUPITA KWENYE MFUMO WA UBADILISHANAJI HUNDI (CLEARING HOUSE)

Kuanzia tarehe 01 Machi 2009, hundi zote ambazo zina thamani ya zaidi ya Shillingi Milioni Kumi (10,000,000.00) hazitaruhusiwa kupita katika mfumo wa Ubadiishanaji Hundi (clearing house) ulioko Benki Kuu Dar es Salaam pamoja na matawi yake yote nchini. Malipo yoyote yanayozidi Shilingi Milioni Kumi (10,000,000) yafanyike kwa kupitia mfumo wa Malipo wa Taifa uitwao 'Tanzania Interbank Settlement System (TISS)'.

Hundi za Serikali zenyе thamani ya zaidi ya Shillingi za Kitanzania Milioni Kumi (10,000,000.00) zitaendelea kupokelewa kama kawaida katika mabenki ya biashara na kupitishwa kwenye mfumo huo wa ubadiishanaji mpaka hapo itakapotangazwa vinginevyo.

Mabenki yote yanashauriwa kuendelea kutoa elimu ya mabadiliko haya kwa wateja wake ili kupunguza usumbufu unaoweza kujitokeza.

Wadau wote wanaombwa kuzingatia mabadiliko haya.

(Imesainiwa)

Gavana

20 Februari 2009

